

## MAKAO MAKUU, DODOMA

# \*DC apongeza Bodii ya Maziwa kusaidia wenyewe mahitaji

**M**KUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobasi Katambi amepongeza Bodii ya Maziwa kwa kusaidia maziwa kwa wahitaji wasiokuwa na uwezo ili kurejesha nuru ya afya zao.

Mkuu huyo alitoa pongezi hizo wakati akipokea lita 1,650 za maziwa kutoka Bodii ya Maziwa

kwa ajili ya watoto wa Kituo cha Kijiji cha Matumaini, Kituo cha Afya cha Mkonze, Chigongwe na Hospitali ya Mkoa.

Katambi alisema bodii hiyo imefanya jambo zuri la kutoa maziwa hayo kwani yatasaidia kuw-tengenezea lishe watoto wa Kijiji cha Matumaini na katika vituo vya afya na hospitali ambazo zimepata mgao huo.

Alisema kampuni ambazo zimefanya hilo zinas-tahili pongezi kutokana kuonesha kwamba nao wanahuksika na ulezi wa jamii wakiwemo watoto na wagonjwa.

"Naomba kampuni nyingine ziige mfano huo, tunahitaji kuona watoto walio katika mazingira magumu wanatunzwa kwa kupewa vyakula vya lishe," alisema.

Naye Padri Vicent kutoka Kijiji cha Matumaini aliishukuru Bodii ya Maziwa na serikali kutokana na kutoa msaada huo kwa watoto waliopo katika kijiji hicho.

Alisema serikali kupitia taasisi zake imekuwa ikiwakumbuka mara kwa mara watoto yatima ambao wanatunzwa katika vituo mbalimbali vya malezi.

